# Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia Siku 16 za Kampeni: **Uwasilishaji wa Mada kwa kutumia Power Point**

## Utangulizi

Wakati wa Siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia , wanachama wote wa Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia watatoa wito kwa viongozi kuonyesha uongozi wao kwa kutambua Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana kama ukiukwakaji wa haki za binadamu na kikwazo kwa maendeleo ya kijamii , kiuchumi n.k. Tunatoa wito kwa watendaji wa serikali, baraza la mawaziri, wabunge, viongozi wakuchaguliwa katika ngazi mbalimbali za serikali , viongozi wa kimila / kitamaduni na dini kwa:

- Kulaani hadharani Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana
- Kutengeneza mpango mkakati wa taifa wa kuzuia na kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Wanawake
- Unganisha nguvu na taasisi na mfumo wa uratibu wa taifa wa kusimamia juhudi za kitaifa
- Kuhakikisha mgawanyo wa bajeti ya kutekeleza mpango mkakati wa Taifa

Shughuli mojawapo ya ufanisi wa kushirikisha viongozi ni mikutano ya utetezi. Mikutano hii inaweza kutumika kwa kugusia suala la Ukatili Dhidi ya Wanawake na athari zake kwa maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kutoa wito kwa viongozi kuchukua hatua ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana. Maelezo hapa chini na uwasilishaji wa mada kwa Power Point unatoa mwongozo kwa asasi kuwezesha mikutano ya utetezi kwa viongozi wao.

## Jinsi ya uwasilishaji mada kwa Power Point

- Maelezo haya yanahusiana na uwasilishaji wa mada kwa Power Point zilizotolewa katika kifurushi cha kuchukua hatua na utetezi.
- Inatoa maelekezo ya kuongoza mada yako.
- Soma maelezo haya kwa kina kabla ya kutumia uwasilishaji mada kwa Power Point.
- Tumia karatasi ya kazi iliyotolewa katika kifurushi cha kuchukua hatua na utetezi na uzibalishe ili kulingana hizi dondoo za uwasilishaji mada za Power Point yaani kujaza baadhi ya taarifa maalum za nchi (maelekezo yametolewa katika maandishi ya italiki ndani ya waraka huu na katika uwasilishaji mada wa Power Point).

## Maelezo ya uwasilishaji.

### Ukatili Dhidi ya Wanawake.

Umoja wa Mataifa umefafanua Ukatili Dhidi ya Wanawake kama “kitendo chochote cha ukatili wa kijinsia kuwa ni matokeo, au ni uwezekano unao sababisha, madhara ya kimwili, kingono au kiakili / kisaikolijia au mateso kwa wanawake, ikiwa ni pamoja na vitisho vya vitendo hivyo, kutumia nguvu au kunyimwa uhuru , vinaweza kufanyika kwa uwazi au kwa siri katika maisha ya mtu binafsi. “



GBV PREVENTION NETWORK
Building Momentum•Fostering Activism

## Ukubwa wa tatizo la Ukatili dhidi ya Wanawake.

Ukatili Dhidi ya Wanawake ni janga la kimataifa ambapo 1 kati wanawake 3 hufanyiwa ukatili katika maisha yao.

Katika Afrika asilimia 36.6 ya wanawake hupatwa na ukatili wa kimwili na / ukatili wa kingono kutoka kwa mwenzi wake. Karibu asilimia 11 ya wanawake katika bara la Afrika wamefanyiwa ukatili wa kingono na watu wasio wenzi wao. Inakadiriwa kuwa karibuni wasichana na wanawake milioni 100-140 wamefanyiwa ukeketaji, wakati wasichana zaidi ya milioni 3 katika Afrika wako katika hatari ya kufanyiwa ukeketaji kila mwaka, na takriban wasichana milioni 70 duniani kote wameolewa kabla ya umri wa miaka 18, wengi wao kwa ndoa za kulazimishwa.

Katika Ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika, asilimia 38.83 ya wanawake ambao wamekuwa katika mahusiano wamefanyiwa ukatili na wenzi wao wa ndani katika Afrika ya Mashariki, na asilimia 29.67 Kusini mwa Afrika. Makadirio ya kiwango cha matukio ya unyanyasaji wa kijinsia kutoka kwa wasio wenzi wao ni asilimia 11.4 katika Afrika Mashariki na asilimia 17.4 kwa Kusini mwa Afrika.

**(Tafadhali ingiza takwimu za kitaifa za Ukatili Dhidi ya Wanawake katika nchi yako- hii inaweza kupatikana kutoka kwenye Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya au WHO taarifa ya tathmini duniani juu ya Afya au tafiti nyingine za kisayansi kitaifa).**

### Athari na Gharama za Ukatili dhidi ya Wanawake na Wasichana.

Kuna madhara mbalimbali ya ukatili, ikiwa ni madhara ya mara moja, muda mfupi na muda mrefu. Yana athari kwa mtu binafsi, familia, na jamii kwa ujumla wake, ambayo huleta athari katika ngazi ya taifa,kanda na kimataifa. Athari hizo zinajumuisha yafuatayo:

**Ukatili Dhidi ya Wanawake unapunguza uzalishaji na kuongeza rasilimali kwenye bajeti ya Taifa.** Ina gharama kubwa moja kwa moja au isiyokuwa moja kwa moja kwa wahanga, waajiri na sekta ya umma katika suala la afya, polisi, sheria na matumizi yanayohusiana vilevile na upotevu wa mishahara na uzalishaji.

- Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika nchini Uganda, asilimia 9 ya matukio ya ukatili wa kijinsia husababisha wanawake kupoteza muda wa kuingiza kipato, kwa kiasi cha takriban siku 11 katika mwaka (ICRW, 2009)
- Inakadiriwa hasara ya uzalishaji kutokana na ukatili wa majumbani nchini Tanzania ni asilimia 1.2 (WHO, 2008)
- Gharama ya kila mwaka ya ukatili wa wanamke wanaofanyiwa na mwenzi wao Afrika Kusini, imeigharimu nchi ya Afrika Kusini kiasi cha Randi bilioni 28.4
    - Nchini Uganda, gharama ya kila mwaka ya wafanyakazi wa hospitali katika kuwatibu wanawake wenye majeraha yanayohusiana na Ukatili dhidi ya wanawake waliofanyiwa na wenzi wao ni dola za kimarekani milioni 1.2. (Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Wanawake-ICRW, 2009)
    - Nchini Moroko, gharama za Ukatili dhidi ya wanawake waliofanyiwa na wenzi wao zimeugharimu mfumo wa sheria kiasi cha dola za kimarekani milioni 6.7 kwa mwaka. (ICRW, 2009)

**(Tafadhali ingiza takwimu za kitaifa zinazohusiana na gharama za kiuchumi za Ukatili Dhidi ya Wanawake katika nchi yako).**

**Ukatili wa kingono unanyima wasichana elimu na kupunguza fursa za ukuaji wa maendeleo ya taifa.** Ukatili unaotokea mashuleni unapunguza fursa za elimu na mafanikio kwa wasichana.

- Utafiti uliofanyika nchini Ethiopia, asilimia 23 ya wasichana wameripotiwa kufanyiwa ukatili wa kingono au kubakwa njiani wanapo kwenda au kutoka mashuleni.
- Nchini Afrika Kusini, asilimia 33 ya taarifa ya ubakaji wa wasichana ulikuwa unaofanywa na walimu. Wasichana wengi walihama shule au kuacha shule kutokana na uhasama baada ya kutoa taarifa ya ukatili waliofanyiwa.

**(Tafadhali ingiza takwimu za kitaifa zinazohusiana katika nchi yako).**

**Ukatili unachochea maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI.** Ukatili unapunguza uwezo wa wanawake kujilinda na maambulizi ya Virusi Vya UKIMWI, na wanawake wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI mara nyingi hukutana na unyanyasaji na unyanyapaa. Wasichana wadogo wako katika hatari kubwa ya ukatili wa kijinsia na maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI: Wanawakilisha takriban asilimia 60 ya milioni 5.5 ya vijana wote duniani wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI. Utafiti uliofanyika Tanzania, Rwanda na Afrika Kusini unaonyesha kwamba wanawake waliofanyiwa ukatili na wenzi wao wanauwezekano mkubwa wa kuambukizwa Virusi Vya UKIMWI kulinganisha wale ambao hawajafanyiwa ukatili. Zaidi ya asilimia 14.6 ya wanawake walio kusini mwa jangwa la Sahara Afrika na kusini-mashariki mwa Asia wameripotiwa kwamba wanapojitangaza wanaishi na Virusi Vya UKIMWI, inawapelekea wenzi wao kuwafanyia ukatili. Hofu ya ukatili ni kikwazo kwa wanawake kuweka wazi hali zao na kushindwa kupata huduma sahihi.

**Kwa nini tunazuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.**

- Kuokoa gharama kwa mtu binafsi, familia, jamii na ngazi ya Taifa.
- Kuhamasisha ushiriki sawa wa wasichana na wavulana, wanawake na wanaume katika nyanja za kisiasa na elimu.
- Kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
- Kutimiza ahadi zilizotolewa kwa kuzingatia utu na haki za kila raia kutokana mifumo ya kisheria ya kitaifa na kimataifa.

**Mifumo ya kisheria ya kiutendaji ili kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana.**

Juhudi mbalimbali zimefanyika katika ngazi ya kimataifa, kikanda na kitaifa ili kushughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana. Kuna mifumo kadhaa ya kisheria na kiutendaji ambayo imewekwa ili kuweka mazingira mazuri ya kuzuia na kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Wanawake. Nchi kadhaa katika kanda zimetia saini mifumo hii, kuashiria dhamira yao ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake. Baadhi ya mifumo muhimu ya kisheria na kiutendaji katika ngazi ya kimataifa na kikanda ni pamoja na:

- Mkataba wa kutokomeza aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake (CEDAW) na itifaki zake (1979): Unatambulika kama mswada wa haki za wanawake kimataifa kwa sababu unatambua ukiukwaji wa haki za wanawake wanaofanyiwa na kutoa wito kwa serikali za nchi husika kuchukua hatua maalum kulinda haki za wanawake kama haki za binadamu. Ingawa CEDAW haitamki bayana Ukatili Dhidi ya Wanawake, kamati ya CEDAW hatimaye ilipitisha mapendekezo makuu ya 12 na 19 yaliyojumuisha suala la Ukatili Dhidi ya Wanawake na kutoa mapendekezo ya kina kwa serikali za nchi. Nchi za Sudan, Sudan Kusini na Somalia hawajaridhia CEDAW.

- Tamko juu ya kuondoa Ukatili Dhidi ya Wanawake (DEVAW) hii ilipitishwa na Umoja wa Mataifa mwaka 1993: DEVAW ni waraka muhimu zaidi umetokana na matamko ya Umoja wa Mataifa kuhusu Ukatili Dhidi ya Wanawake. Inashughulikia mifumo ya kitamaduni,kijamii na kwa mtu binafsi ya Ukatili ambao wanawake wanafanyiwa.
- Azimio la Beijing na Jukwaa la utekelezaji: Hili lilipitishwa mwaka 1995 katika mkutano wa dunia wa nne wa wanawake. Tamko la utekelezaji lilihusisha suala la Ukatili Dhidi ya Wanawake kama moja ya maeneo muhimu ya kushughulikiwa. Pia ilitambua maeneo maalum ya utekelezaji kwa serikali kuchukua hatua, kuzuia na kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana.
- Azimio la Vienna na Programu ya Utekelezaji ya 1993: Hii ilipitishwa katika makubaliano ya wawakilishi wa nchi 171 katika mkutano wa dunia wa Haki za binadamu katika mji wa Vienna. Inasisitiza hadhi sawa na haki za wanawake na inatetea haki za wanawake na wasichana kulindwa.
- Mkutano wa Kimataifa wa Idadi ya Watu na Maendeleo wa 1994: Moja ya kanuni za msingi ambazo PoA inahusika (kanuni 4) inaweka wazi na kulenga haki za binadamu kuwa ni haki za wanawake na inasisitiza haja ya usawa wa kijinsia. Inatetea kuondoa kila aina ya Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana na inasema haja ya kuwapa uwezo wa kudhibiti uzazi wao.
- Itifaki ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na za Watu kuhusu Haki za Wanawake barani Afrika: Itifaki hii ilianza kutumika mnamo mwaka wa 2005 na ni chombo cha kisheria. Mpaka sasa umeridhiwa na nchi 36 za Afrika. Unajibu hoja za wanawake wa Kiafrika; ambayo haijawahikuwepo mikataba mingine ya kimataifa inayo hakikisha upatikanaji wa haki kwa wanawake katika mapana yake. Pia inatambua haki za wanawake na wasichana kulindwa kutokana na unyanyasaji wa kingono (haki ya usawa katika elimu). Imetoa waraka unaoelezea kuhusu Ukatili Dhidi ya Wanawake na nukuu zake katika waraka mzima.
- Azimio la kuhakikisha kusimamia Usawa wa Kijinsia katika Afrika (2004): Hii ilifanywa na Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika kwenye mkutano uliofanyika nchini Ethiopia mwaka 2004. Viongozi wa Afrika walisaini dhamira yao ya usawa wa kijinsia kama ilivyo ainishwa katika kifungu cha 4 (I) cha Sheria ya Katiba ya Umoja wa Afrika.
- Sera UA ya Jinsia na Mpango wa Utekelezaji (2010): Sera hii "Inatoa mfumo ambao unaharakisha kufikiwa kwa usawa wa kijinsia, haki kati ya wanaume na wanawake, kutonyanyaswa na haki za msingi katika Afrika". Ina nia ya kuharakisha uhuishaji wa masuala ya jinsia, kuwajengea uwezo wanawake na kuwalinda na vitendo vya ubakaji na ukatili.

**Tafadhali ingiza mifumo ya Kisheria na uendeshaji ya kikanda inayotumika kwenye kanda yako, mfano Itifaki ya Jinsia ya SADC, Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki nk. Tafiti na jumuisha taarifa mbalimbali kuhusu mikataba iliyoridhiwa na kusainiwa na nchi yako kama hapo juu, yaani ambayo imeridhiwa na ambayo haijaridhiwa.**

## Mazingira ya Kitaifa ya sheria na sera

**Katika sehemu hii tafadhali tafiti na jumuisha taarifa zifuatazo**

- **Angalia vifungu ndani ya katiba ya nchi yako kuhusu usawa wa kijinsia. Kama hakuna, onyesha pia**
- **Angalia na jumuisha taratibu na kanuni za adhabu katika sheria hiyo vinavyoshughulikia suala la Ukatili Dhidi ya Wanawake**
- **Jumuisha sheria nyingine yoyote, sera na mipango ya kitaifa ndani ya nchi yako vinavyoshughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake**
- **Angalia na jumuisha maendeleo katika utekelezaji wa hayo yaliotajwa hapo juu**

- **Angalia na jumuisha mapungufu katika utekelezaji yaani kukosekana kwa mipango ya utekelezaji, kutokuwepo na bajeti ya kutosha, ukosefu wa maarifa na ujuzi ndani ya taasisi za utekelezaji nk**

Kuongoza njia ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana

Wakati huu wa Kipindi cha Siku 16 tunatoa wito juu yako kuonyesha uongozi kwa:

Ingiza mahitaji yako maalumu ya kampeni za siku 16 (huenda ni pamoja na:. Kulaani hadharani Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana, kuweka mipango mkakati ya taifa yenye ufanisi, kuanzisha mifumo ya uratibu inayojumuisha sekta mbalimbali na bajeti ya kutekeleza mpango mkakati wa taifa)

Tumia sauti yako na uwezo wako kuchukua hatua na kuongoza njia ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana!